

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE.
MAGALULA SAID MAGALULA ALIYOITOA WAKATI WA
UZINDUZI WA WIKI YA SHERIA NCHINI KANDA YA
SUMBAWANGA TAREHE 01 FEBRUARI, 2016**

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi, Kanda ya Sumbawanga,

Mheshimiwa Jaji Kassim M. Nyangarika, Jaji wa Mahakama Kuu
Kanda ya Sumbawanga.

Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Rukwa,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,

Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini,

Mheshimiwa Msajili wa Wilaya, Kanda ya Sumbawanga

Waheshimiwa Mawakili wa Serikali na Wakujitegemea,

Waheshimiwa Mahakimu,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
ya Sumbawanga.

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa Taasisi za Umma na Taasisi binafsi,

Watumishi wa Mahakama,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahala hapa siku hii ya leo.

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Viongozi wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga kwa kunipa heshima ya kuwa “Mgeni rasmi” katika Siku hii adhimu ya Uzinduzi wa Wiki ya Sheria Nchini. “Asanteni sana kwa heshima hii”

Aidha nichukue fursa hii kuwapongeza kwa maandalizi mazuri ya shughuli yetu ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria Nchini “Hongereni sana”

Kutokana na uwepo wa Wadau mbalimbali mahala hapa naona ni vema kupitia ninyi kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Wadau wa Maendeleo ndani ya Mkoa niwashukuru kwa kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015 kwa amani na utulivu mkubwa hata pindi changamoto zilipojitokeza tuliweza kuzimaliza kwa amani.

Hivyo basi katika kipindi hiki cha Mwaka 2016, baada ya shughuli za Uchaguzi kuisha tunawajibika kufanya kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo yetu binafsi na maendeleo ya Mkoa, kwa kushirikiana na Viongozi wetu tuliowachagua kutuongoza bila kuathiriwa na tofauti za kitikadi.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Leo ni uzinduzi wa Kilele cha Wiki ya Sheria Nchini, maadhimisho ambayo kilele chake kitafikiwa tarehe 04 Februari, 2016. Katika kuadhimisha siku ya sheria Nchini mwaka huu tutaongozwa na kauli mbiu isemayo ***“HUDUMA ZA HAKI KUMLENGA MWANANCHI: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU”***

Kauli mbiu hii ni sahihi katika Maadhimisho yetu haya kwa kuwa Mahakama ndiyo chombo pekee ambacho kila Mwananchi na kila Mdau anategemea kupata Haki, pia Mahakama ndiyo Chombo pekee ambacho kipo kwa mujibu wa sheria kutoa Haki. Endapo shauri limeshindwa kuafikiwa katika ngazi nyingine nje ya Mahakama basi shauri hilo linapelekwa Mahakamani.

Wanachi wanakimbilia Mahakamani kwa kuwa wanaamini Haki itapatikana huko na pande zote zinaridhika.

Tafsiri ya haraka ya neno “Haki” ni usawa, isiyo na upendeleo, inayozingatia sheria na isiyo na maslahi ya upande mmoja.

Maadhimisho haya yanatoa fursa kwa Wananchi kutambua huduma za Mahakama ambazo zinazingatia “Haki” yenye tafsiri kuwa haina upendeleo wala maslahi ya upande mmoja.

Hivyo basi tafsiri ya Huduma za Haki kumlenga Mwananchi kwa maana nyingine ni Huduma zote zinazotolewa na Mahakama kwa misingi ya "Haki" ziweze kutolewa kwa Wananchi pindi zinapohitajika.

Uwepo wa chombo cha Mahakama siyo wa bahati mbaya bali ni kukidhi mahitaji ya Jamii ya kupata "Haki". Kila mmoja wetu anapenda kupata kile anachostahili, sasa kutokana na mazingira au kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea za kujiongezea kipato au kutafuta namna bora ya kuishi, kunakuwa na mazingira ya ukiukwaji "Haki" kwa makusudi au kwa bahati mbaya.

Kwa kuwa binadamu anahitaji kuishi, na anaishi katika mazingira mbalimbali na anafanya shughuli mbalimbali, hivyo uwepo wa chombo cha Mahakama moja kwa moja unahalalishwa au haukupukiki "inevitable" kwa kuwa katika kuishi huko Binadamu huyu atahitaji "Haki" ambayo inatolewa na Mahakama kwa mujibu wa Sheria.

Wito wangu kwa Wananchi, chombo hiki cha mahakama kiwe karibu nasi na tukitumie. Katika Ibara ya **107 A** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaeleza kuwa mamlaka yenye kauli ya Mwisho katika Utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mahakama.

Katika ibara ya 107 A (2) kuna mambo ya msingi ya kuzingatiwa katika utoaji wa haki:-

- Kutoa haki kwa watu wote bila kujali hali ya mtu
- Kutochelewesha haki bila sababu
- Kutoa fidia ipasavyo kwa watu walioathirika kwa mujibu wa sheria
- Kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro
- Kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

Tukiendelea kuitizama Kauli mbiu yetu, tunaona neno ***“Wajibu wa Mahakama na Wadau”***

Mbali na Mahakama tunaona wapo wadau wengine ambao kwa sehemu wanayo nafasi katika kupelekea Haki kupatikana, katika Wadau hao tunaona wapo Makama wenyewe, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Taasisi za Haki za Binadamu na masuala ya sheria, Vyama vya Wanasheria, Kampuni za Uwakili, Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, Pia hapo wapo Wadau muhimu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Palipo na mafanikio hapakosi changamoto, katika kuhakikisha Haki inatendeka Mahakama na Wadau tuna wajibu wa kutekeleza majukumu yetu ipasavyo kwa kuzingatia maadili na mkataba wa huduma kwa Mteja.

Kila mdau pindi anapotimiza majukumu yake ipasavyo atapelekea, Taasisi nyingine hivyo hivyo kutimiza wajibu wake ipasavyo na kupelekea "Haki" kutendekeza, inawezekana baadhi ya Wadau sikuweza kuwaainisha katika orodha niliyoitaja ya Wadau ambao kwa kushirikiana na mahakama wanaweza kupelekea "Haki" kutendeka kwa wakati na kumlenga Mwananchi.

Naomba tuzidishe ushirikiano na tuongeze ukaribu katika utendaji kazi tukimlenga Mwananchi ambaye ndiye Mdau Mkuu katika utoaji wa "Haki"

Napenda kuhitimisha kwa kuwashukuru Wadau wote ambao mmeweza kushiriki nasi mahala hapa, Nawashukuru Watumishi wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga, Nawashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wengine wote ambao mmeweza kufanya maandalizi ya shughuli yetu hii ya leo

Tudumishe umoja miongoni mwetu, Mkoa wetu una changamoto nyingi katika kujiletea maendeleo, penye Umoja pia "Haki" ipo

Asanteni kwa kunisikiliza

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Nchini yamezinduliwa rasmi

Magalula S. Magalula
MKUU WA MKOA RUKWA